



KIBABII UNIVERSITY

UNIVERSITY EXAMINATIONS

2021/2022 ACADEMIC YEAR
FIRST YEAR SECOND SEMESTER

MAIN EXAMINATION

FOR THE DEGREE OF MASTER OF ARTS IN KISWAHILI

COURSE CODE: SWA 817

COURSE TITLE: ISIMU JAMII

DATE: 25/05/2022

TIME: 2:00PM-4:00PM

MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee. Kila swali lina alama 20.

MUDA: Masaa Matatu (3)

KIBU observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

10

Maswali

1. a) Tofautisha lugha na lahaja kwa kutumia vigezo vitatu.
b) Kwa kutumia mifano faafu kutoka lugha za Kenya chambua vipengele vinavyotofautish lugha za kibantu na kinile.
c) Kwa kurejelea matumizi ya lugha nchini Kenya, tathmini iwapo dhana *lugha ya mama* bado inafiki kurejelea lugha ya kwanza anayopokea mtoto kwa minajili ya mawasiliano.

(alama 20)

2. Dadavua kwa kutumia mifano aina tano za matokeo ya migusano na mitagusano ya lugha.

(alama 20)

3. a) Pambamua aina tatu za upangaji lugha.
b) Tathmini sababu zinazofanya nchi kupanga lugha.
c) Kwa kurejelea nchi za Kenya, Somalia na Tanzania baada ya uhuru, bainisha jinsi amri za viongozi wa nchi hizi zilivyo nguzo muhimu katika ukusaji wa Kiswahili na Kisomali kuwa lugha rasmi na lugha za taifa.

(alama 20)

4. a) Jadili mifanano na tofauti za vipimo vifuatavyo vya uhai wa lugha
i) Kipimo cha UNESCO cha uhai na tishio la kufa kwa lugha
ii) Kipimo cha Fishman (1991) cha utatizaji wa lugha kihatua kizazi hadi kizazi
b) Pambanua jinsi utakavyotumia vipimo hivi viwili kupima uhali wa lugha ya yote asilia nchini Kenya.

(alama 20)

5. Tathmini ufaafu wa nadharia za uchopekaji na muktadha katika uchambuzi wa matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali na tafiti za kiisimu jamii. (alama 20)